


TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.02 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz



BIMA
Ni Kinga,
Leo na Kesho!

Uhakika wa Matibabu ni Kuwa na Bima ya Afya!

Yaliyomo

01



08



Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma

Mhariri
Hadija Maulid

Waandishi
Tabia Mchakama
Anna Massao

Msanifu
Abubakari W. Kafumba

TIRAUpdates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRAUpdates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Januari 2025.

01

TIRA na Wadau Wake Wakabidhi Hundi ya Milioni 321 Kuunga Mkono Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar

02

Wafanyakazi TIRA Wakumbushwa Uwajibikaji, Uledi na Uwazi ili Kuleta Ufanisi katika Sekta

04

"Wananchi mna wajibu na Haki ya Kukata Bima, Kata Bima Kulinda Afya, Mali na Uwekezaji" – Dkt. Saqware

06

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Yachochea Upatikanaji wa Huduma za Matibabu Nchini

08

Mapinduzi ya Miaka 61 ya Zanzibar na Ukuaji wa Sekta ya Bima visiwani humo

10

PIC Yaridhishwa na Utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania

12

Dkt. Jafo Asisitiza Miradi ya Kimkakati Kukatiwa Bima na Kampuni za Ndani

13

Kamishna wa Bima Tanzania Akutana na Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB

14

Utoaji Elimu ya Bima kwa Umma: TIRA Yashiriki Wiki ya Sheria 2025

16

Ukurasa wa Kamishna

17

Matukio Kwenye Vibango



Scan
Kusoma Kidijiti




Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
info@tira.go.tz

Au
Piga simu bure +255 222 132 537

Tovuti yetu
www.tira.go.tz

TIRA na Wadau Wake Wakabidhi Hundi ya Milioni 321 Kuunga Mkono Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania TIRA na wadau wake hapo Januari 7, 2025 wamekabidhi hundi ya mfano ya shilingi milioni 321 kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla ikiwa ni mwendaji wa Sekta ya Bima nchini kuunga mkono Maadhimisho ya 61

ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo kilele chake kilikua ni tarehe 12 Januari 2025 Gombani Stadium, Pemba.

Naibu Kamishna wa Bima Tanzania, Bi. Khadija Said aliongoza ujumbe uliokabidhi hundi hiyo ameeleza kuwa hatua hii ni utekelezaji wa ahadi ya

sekta ya bima nchini ya kuwa sehemu ya maadhimisho hayo ili kuibua na kuchochea ushirikiano wenye tija na Serikali hususani kwenye miradi mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa hapa nchini kuona namna kampuni za bima za nchini zinavyoweza kushiriki

kwenye kuingia majanga.

Katika ujumbe huo pia Mwakilishi wa Umoja wa Kampuni za Bima Tanzania (ATI) Bw. Wilson Mnzava ambae pia ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya CRDB (CIC) ameishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikisha



Kampuni za Bima katika tukio hilo muhimu, amesema” huu ni mwanzo tu tunaahidi kwamba tutaendelea kushiriki kila mwaka ili kuhakikisha kwamba sekta ya bima nchini inakua ni miongoni mwa mafanikio ya maadhimisho haya”.

Aidha, Bw. Wilson ameiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoa fursa kwa kampuni za bima za nchini ili ziweze kushiriki kwenye kukinga

miradi mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa nchini ya serikali na wawekezaji binafsi.

Akipokea hundi hiyo Mhe. Hemed Suleiman Abdulla ametoa shukrani za dhati kwa sekta ya bima nchini kwa hatua hii akisema,”mchango huu ni mkubwa na tunauthamini.

Fedha hizi mlizochanga zitatumika kama ilivyokusudiwa.

Tuendeleo kufanya kazi kwa juhudi tukiwa na matarajio kuwa kazi inayofanyika kwenye sekta ya bima nchini ni kwa ajili ya Watanzania na kuleta ushirikiano wenye tija, natoa wito kwa kampuni za bima nchini kuchangamkia fursa za Biashara zilizopo na ofisi yangu ipo tayari kutoa msaada pale inapohitajika”.

Wafanyakazi TIRA Wakumbushwa Uwajibikaji, Uledi na Uwazi ili Kuleta Ufanisi katika Sekta

no wa Pili wa Baraza la Nne la Wafanyakazi 2025

aulimbiu: “Bajeti Shirikishi kwa Soko Salama la Bima”



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) wameaswa kuendelea kuzingatia ueledi, uwajibikaji, na uwazi ili kuhakikisha sekta ya bima inazidi kuimarika na kuchangia maendeleo ya taifa.

Hayo yameelezwa na Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Pili wa Baraza la Nne la

Wafanyakazi kwa mwaka 2025 uliofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili kuanzia, tarehe 30 Januari 2025 hadi tarehe 31 Januari 2025.

Dkt. Saqware alisisitiza umuhimu wa kutoa huduma bora kwa wateja huku akihimiza umuhimu wa kuendeleza ushirikiano kazini.

“Kipimo cha utoaji wa huduma bora kinaanzia

hapa kazini baina yetu wafanyakazi. Hudumianeni vizuri kwani Wafanyakazi wote TIRA tunategemeana ili kuleta ufanisi.”

Mkutano huo umewakutanisha wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi kutoka ofisi mbalimbali za kanda, ukiwa na lengo la kujadili na kupitisha bajeti pamoja na masuala mengine muhimu yanayohusu utendaji wa TIRA.

Pamoja na majadiliano ya bajeti, mkutano huo pia umeleta fursa ya mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi wa TIRA, yenye lengo la kuwajenga uwezo ili kuwahamasisha na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija kubwa katika sekta ya bima na hatimaye kufikia malengo yaliyowekwa.

“Wananchi mna Wajibu na Haki ya Kukata Bima, Kata Bima Kulinda Afya, Mali na Uwekezaji” – Dkt. Saqware

Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware ashiriki kutoa elimu ya bima kwenye kipindi cha Pambazuka kilichorushwa na Redio One, Januari 23, 2025.

Katika mahojiano hayo Kamishna alitoa elimu na ufafanuzi wa mambo mbalimbali yanayohusu bima, na kusisitiza wajibu na haki ya kila Mwananchi katika soko la bima, lakini pia alijibu maswali ya wasikilizaji waliouliza kwa njia ya simu.

Kamishna alianza kwa kuelezea aina za bima, umuhimu wa bima akisisitiza kuwa bima ipo kwa ajili ya kulinda mali, afya na uwekezaji hasa pale yanapotokea majanga ili mwathirika aweze kurudi katika hali yake ya kawaida.

Dkt. Saqware pia alisisitiza umuhimu wa kukata bima kwa wananchi “Sisi Mamlaka ya Usimamizi wa Bima tunawakumbusha wananchi kuwa mna wajibu na haki kwa kila jambo ikiwemo kukata bima. Pindi unapopatwa na janga hakikisha kwamba unatoa taarifa sahihi na ili kuendana na fidia unayostahili kupata, pia hakikisha una viambatisho

vyote ili kuwezesha kupata stahiki yako kwa uharaka”.

Aidha, alibainisha Mamlaka ni chombo huru ambacho kipo kwa mujibu wa Sheria na kipo kwa ajili ya kutatua changamoto za wananchi.

Kuhusu Bima ya Afya kwa Wote Kamishna alieleza kuwa TIRA imeanza kuzisimamia skimu mbalimbali za bima hizo ikiwemo NHIF.

Kwa upande wa ulipaji wa madai Kamishna ameeleza kuwa asilimia 95 ya madai ya bima yanalipwa kwa wakati na kwa usahihi hivyo alisisitiza kila mwananchi akikata bima anapaswa kulipwa fidia pale anapopatwa na majanga.

Lakini pia alishauri Mwananchi kufika ofisi za Mamlaka iwapo ana malalamiko kuhusu bima.

Kamishna wa Bima Tanzania, alimalizia mahojiano hayo kwa kutoa rai kwa wananchi na watoa huduma za bima kwamba Bima inalipa na hakuna kisichobimika kwani kuna watoa huduma zaidi ya 1500 nchi nzima kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali.





Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Yachochea Upatikanaji wa Huduma za Matibabu Nchini



Kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kutaongeza mchango wa sekta ya bima katika kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za matibabu kupitia mfumo wa bima ya afya. Hayo yalibainishwa wakati Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama, alipozindua rasmi Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa

Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) tarehe 21 Januari 2025, jijini Dodoma.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Jenista Mhagama alisema: "Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amemaliza kazi yake ya kuwekeza katika huduma za matibabu. Sasa kazi yenu ni kuhakikisha

wananchi wanatumia huduma hizo kupitia bima ya afya. Ni matarajio yangu kuwa bodi hii mtasimamia jukumu hili kwa nguvu zote."

Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, aliyehudhuria uzinduzi huo, alieleza jinsi sekta ya bima ilivyo chukua

hatua katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za matibabu kupitia mifumo ya bima.

Aidha, sekta ya bima nchini imeendelea kuimarika kwa



kasi, ambapo mchango wake katika pato la taifa umefikia asilimia 2.01 kufikia mwaka 2023. Wanufaika wa huduma za bima, wakiwemo wale wa bima ya afya,

wameongezeka hadi kufikia milioni 23, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 29 kwa mwaka ukilinganisha na miaka ya nyuma. Pia, idadi ya watoa huduma za bima

imeongezeka kwa asilimia 24 kufikia mwaka 2024. Kwa muktadha huu, ni dhahiri kuwa sekta ya bima iko mstari wa mbele katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa watoa huduma za bima ya afya wanawafikia Watanzania wote, na hivyo kuchochea upatikanaji wa matibabu bila vikwazo vya kifedha.

Mapinduzi ya Miaka 61 ya Zanzibar na Ukuaji wa Sekta ya Bima Visiwani Humo



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 sheria ya bima sura ya 394. Pamoja na majukumu mengine imepewa mamlaka ya kuratibu maswala yote ya kisera kuhusu bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi zake za Makao makuu ni Dodoma lakini pia ina Ofisi ndogo Dar es Salaam na Zanzibar.

TIRA ina majukumu

mbalimbali yakiwemo kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima, kuandaa na kutoa miongozo kwa watoa huduma za bima, kusimamia soko la bima nchini, kutoa elimu ya bima, kulinda haki za wateja wa bima, na kuishauri serikali kuhusu masuala ya bima.

Kwenye Maadhimisho ya miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, TIRA ilishiriki

Maonesho ya 11 ya Kimataifa ya Biashara visiwani Zanzibar katika viwanja vya Fumba Dimani kuanzia tarehe 1 Januari 2025 hadi tarehe 15 Januari, huku kilele chake kikiwa Januari 12, 2025 Maadhimisho ya Mapinduzi TIRA imewakilishwa na Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware, Naibu Kamishna wa Bima Bi. Khadija Said na Meneja wa Kanda ya Pemba ambapo Mgeni Rasmi alikua ni Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Saluhu Hassan.

Kupitia Ofisi ya Zanzibar iliyopo Unguja ambapo pia ndipo ilipo ofisi ya Naibu Kamishna wa Bima Tanzania, imeweza kufanikisha mambo mbalimbali yanayoashiria ukuaji wa soko la bima visiwani humo.

Kuimarishwa kwa mifumo ya bima TIRA Zanzibar



imeweza kuboresha mifumo yake ambapo imeongeza urahisi katika usajili kwa watoa huduma lakini pia mifumo hiyo inaisaidia Mamlaka kuhakikisha watoa huduma wanalipa ada zao.

Kufunguliwa kwa ofisi ya TIRA Pemba imesaidia kuhakikisha kuwa idadi ya watazania wanaofahamu kuhusu bima na kutumia bidhaa hizo inaongezeka.

“Uelewa wa bima hapa Pemba unaongezeka siku hadi siku na wananchi wamekuwa na mwamko wa kutaka kufahamu namna bima inavyoweza kuwasaidia wakati wa majanga na fursa

wanazoweza kuzitumia katika sekta hii kuongeza kipato chao” alisema Meneja awa TIRA Pemba Bw. Sharif Hamad.

Aidha, katika Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mwaka 2023 ilieleza ongezeko la Ada za Bima (Gross Premiums Written - GPW) ambazo zimepanda kwa asilimia 7.4 hadi kufikia TZS trilioni 1.24, kutoka TZS trilioni 1.17, watoa huduma za bima wameongezeka kwa asilimia 34, na kufikia 1,549 ikilinganishwa na 1,164 mwaka uliopita.

Aidha, madai ya bima yaliyolipwa yameongezeka kwa asilimia 25.5, hadi kufikia TZS bilioni 488.2

kutoka TZS bilioni 389. Kiwango cha mali za bima kimeongezeka kutoka TZS trilioni 1.7 hadi kufikia TZS trilioni 2.15 huku uwekezaji pia ukiongezeka hadi TZS trilioni .127 kutoka TZS trilioni 1.17.

Fursa za ajira zimeongezeka kwa asilimia 34.1, ambapo jumla ya ajira 5,595 zimerekodiwa mwaka 2023. Aidha, kiwango cha ubakizaji wa bima za kawaida (general insurance retention) kimeongezeka kutoka asilimia 49.4 hadi asilimia 55.5 huku kiwango cha ubakizaji wa bima za maisha kikiwa ni asilimia nah ii ni kwa Tanzania bara na visiwani. Ongezeko la Utoaji Elimu, Ofisi ya

Mamlaka Zanzibar, imeongeza ushiriki wake katika maonesho kama, Siku ya Bima Zanzibar na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ambapo Mamlaka inatoa elimu kwa wananchi mbalimbali wanaotembelea, pia kupitia ushiriki katika vyombo vya habari kama Televisheni, radio na magazeti wakazi wa Zanzibar hufikiwa katika utoaji elimu.

TIRA imeshiriki Maonesho ya 11 ya Kimataifa ya Biashara kama njia ya kukutana na wadau wake mbalimbali, kutoa elimu na kusikiliza changamoto mbalimbali za kibima ambazo zilipatiwa majibu ya moja kwa moja.

PIC Yaridhishwa na Utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania



Kamati ya kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji kwa Umma (PIC) imeridhishwa na utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania- TIRA na kusema kuwa Mamlaka toka kuanzishwa kwake imekua ikiendelea kukua kila mwaka bila kutererika mbali ya kuwa ni Taasisi ya Serikali inayojiendesha yenyewe kwa asilimiamimoja.

Hayo yameelezwa Januari 9, 2025 Bungeni jijini Dodoma na Mkt. wa PIC

Mhe. Augustine Vuma Holle - Mbunge wa Kasulu Vijijini wakati akichangia taarifa ya Utendaji wa TIRA iliyowasilishwa mbele ya PIC. Mhe. Holle ameendelea kusema kuwa taarifa ya utendaji wa TIRA inaonesha wazi kuwa taasisi hiyo imejipanga kutekeleza majukumu yake ipasavyo na hivyo kuwataka TIRA kuendelea kusimamia watoa huduma za bima kwa uthabiti zaidi ili kuendelea kuleta tija kwa wananchi na serikali kwa jumla.

Akitoa taarifa ya utangulizi kwa PIC Mkt. wa Bodi ya Taifa ya Bima CPA. Moremi Marwa amesema kuwa Bodi ya Taifa ya Bima inaendelea kuisimamia Mamlaka ili kuhakikisha kuwa inaendelea kutimiza wajibu wake kama ilivyokusudiwa na Serikali na kusema kuwa kwa ujumla Bodi inaridhika na kiwango cha utendaji wa TIRA ambao umewezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali mathalan mchango wa bima kwa taifa umefikia asilimia 2.01

kwa mwaka wa 2023 ikilinganishwa na asilimia 1.99 kwa mwaka 2022. CPA Moremi Marwa amemaliza kwa kusema kuwa mafanikio yote hayo yamechangiwa na mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara na sera nzuri zinazotekelezwa na Serikali na Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Awali Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware, alieleza mbele ya PIC kuwa Kwa mwaka 2023 takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 69.6 ya kampuni za bima nchini zinamilikiwa na Watanzania. Hali hi inayoonesha kuwa watanzania wanashiriki kuwekeza katika Sekta ndogo ya bima hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wanchi. Vilevile Kamishna alieleza kuhusu majukumu ya TIRA, hali ya ukuaji wa sekta, uandikishaji wa ada za bima na malipo ya fidia za bima ambapo maeneo yote hayo yanaonesha ukuaji wa sekta ya bima.

Akikitimisha wasilisho lake Kamishna wa Bima amesema kuwa Mamlaka chini ya usimamizi wa Bodi ya Taifa ya Bima itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwenye Sekta ya Bima kwa



ajili ya kuendeleza na kusimamia Soko la Bima kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayowekwa na Serikali. Aidha, Mamlaka

itaendelea kuimarisha usimamizi ili kuhakikisha kuwa Soko la Bima nchini linaendelea kuwa salama, endelevu, lenye ushindani na tija kwa maendeleo ya

nchi kwa ujumla.

Nao kwa upande wao Waheshimiwa Wajumbe wa PIC wameitaka TIRA kuendelea kuweka

mazingira yenye usawa wa ufanyaji wa biashara baina ya kampuni na watoa huduma wote wa bima nchini.

Dkt. Jafo Asisitiza Miradi ya Kimkakati Kukatiwa Bima na Kampuni za Ndani



Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Selemani Jafo amesisitiza kuwa Miradi ya kimkakati inayoendelea nchini ikatiwe bima na kampuni za bima za ndani ya nchi ili kukuza sekta ya bima nchini.

Waziri Jafo alisema hayo tarehe 5 Januari 2025 alipotembelea Banda la Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika Maonesho ya 11 ya Kimataifa ya Biashara

Zanzibar yanayoendelea kwenye Viwanja vya Dimani Fumba kuanzia Januari 1 – 15 ambapo ilikua kilele cha uzinduzi rasmi.

“TIRA kama Mamlaka ili kukuza Sekta ya Bima nchini Tanzania Bara na Visiwani, hakikisheni Miradi yote ya Serikali ya Kimkakati inakatiwa bima na kampuni za bima za ndani ili kubakisha Fedha nchini na hii itasaidia

kupanua wigo katika Sekta ya bima” alisema Dkt. Jafo ambaye ndiye Mgeni Rasmi kwenye uzinduzi huo.

Aidha, Bi. Awanje Matenda Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Unguja ambaye amemuwakilisha Naibu Kamishna wa Bima Bi. Khadija I. Said alimueleza Mhe. Waziri kuwa TIRA ina Majukumu ya kusajili, kusimamia na kuendeleza soko la bima nchini, na pia kubainisha

mikakati inayoendelea katika soko la bima kwa sasa. Alimueleza Mhe. Waziri pia kuhusu majukumu ya Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania ambao wanafanya kazi bega kwa bega na TIRA katika kukuza sekta hiyo.

Mamlaka inashiriki maonesho haya kama muendelezo wa utoaji elimu na uhamasishaji kuhusu matumizi ya bima.

Kamishna wa Bima Tanzania Akutana na Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB



January 29, 2025, Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware allitembelea Makao Makuu ya NMB Jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo

na Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo Bi. Ruth Zaipuna kuhusu namna bora ya kuendeleza sekta ya bima nchini hususan Benki Wakala wa Bima (Banc

Assurance).

Akielezea madhumuni ya ziara hiyo Dkt. Saqware amesema Benki wakala bado wana fursa nzuri ya

kupanua wigo wa biashara katika sekta ya bima kwa kubuni huduma mpya mbalimbali hivyo kuwasihi NMB kufanya tafti za Mara kwa mara ili kuona maeneo ya kuboresha.

Kamishna pia aliipongeza NMB kwa kutekeleza vyema mkakati wake wa uhamasishaji matumizi ya bima kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo kampeni maalum.

Katika mazungumzo hayo Bi. Zaipuna aliambatana pia na Afisa Mkuu wa Benki Wakala wa NMB Bw. Martine Massawe ambae aliishukuru Mamlaka kwa ushirikiano na Usimamizi mzuri wa sekta huku akiomba Mamlaka kuendelea kuweka mazingira mazuri ya ya ufanyaji kazi wa benki wakala huku akibainisha namna NMB inavyowekeza kwenye kutoa elimu na kuwafikia umma wa Watanzania ambao ndiyo walengwa wakubwa.

Utoaji Elimu ya Bima kwa Umma: TIRA Yashiriki Wiki ya Sheria 2025



Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yalifunguliwa rasmi Januari 25, 2025 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam na kumalizika Januari 31 2025. Mhe. Sixtus Mapunda, mkuu wa wilaya ya Temeke, akimuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alifungua rasmi maadhimisho hayo, yakiwa na lengo la kukutanisha taasisi mbalimbali kutoa elimu na huduma hasa

zinazohusu sheria.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) ilishiriki maadhimisho hayo kwa lengo la kufikisha elimu ya bima kwa jamii, kutoa ufafanuzi wa sheria za bima na kusikiliza changamoto za kibima kutoka kwa wananchi. Ambapo maafisa mbalimbali kutoka Mamlaka walitoa elimu. Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya "Tanzania ya

2050, nafasi ya Taasisi zinazosimamia haki madai katika kufikia malengo makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo".

Meneja wa Sheria na Kushughulikia Malalamiko Bw. Okoka Mgavilenzi alitoa elimu ya bima kwa Mkuu wa Wilaya na wadau walioshiriki ambapo alieleza kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka, majukumu yake na kuhusu sheria

mbalimbali zinazosimamia soko la bima nchini zikiwemo Sheria za Bima ya Afya kwa Wote Na. 13, ya mwaka 2023, ambapo Mamlaka imepewa jukumu la usimamizi na Mhe Mapunda alitoa rai kwa Mamlaka kuendelea kufanya kazi kwa ueledi na uwajibikaji akisisitiza yeye pia ni mnufaika wa kulipwa madai ya kibima hivyo TIRA ipo kutatua kero za wananchi.

Ukurasa wa Kamishna

UKURASA WA KAMISHNA WA BIMA

Mafanikio na mabadiliko katika sekta ya bima mwaka 2024

Hadja Maulid, Meneja Uhusiano na Mawasiliano-TIRA

Mpendwa msomaji, karibu katika ukurasa maalumu wa Kamishna wa Bima Tanzania, ambapo leo Kamishna anazungumzia mafanikio na mabadiliko katika sekta ya bima mwaka 2024, endelea:

Mwaka 2024 umekuwa wa mafanikio na mageuzi makubwa kwa sekta ya bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ikijidhihirisha kama kiongozi wa mabadiliko hayo kwa usimamizi na ushirikiano wa karibu na wadau wa sekta, TIRA imechukua hatua madhubuti za kuimarisha soko la bima, kuboresha mifumo, na

kuongeza uelewa wa bima miongoni mwa Watanzania.

Uzinduzi wa taarifa ya utenda wa soko la bima kwa mwaka 2023

Tukio hili lilifanyika mwezi Novemba 2024 na kuhudhuriwa na watu zaidi ya 400 huku watu zaidi ya 1000 wakifuatilia mbashara kupitia mtandao wa YouTube wa mamlaka. Taarifa hii imeonesha kukua kwa soko kwa kiwango kikubwa kama ifuaavyo;

Ada za Bima (Gross Premiums Written - GPW) zimepanda kwa asilimia 74 hadi kufikia Sh 1.24 trilioni kutoka Sh 1.17 trilioni, watoa huduma za bima wameongezeka kwa asilimia 34, na kufikia 1,549 ikilinganishwa na 1,164 mwaka uliopita. Aidha, madai ya bima yaliyolipwa yameongezeka kwa asilimia 25.5, hadi kufikia Sh 488.2 bilioni kutoka Sh 389 bilioni.

Kiwango cha mali za bima kimeongezeka kutoka Sh 1.7 trilioni hadi kufikia Sh 2.15 trilioni huku uwekezaji pia ukiongezeka hadi Sh 1.27 trilioni kutoka Sh 1.17 trilioni. Fursa za ajira zimeongezeka kwa asilimia 34.1, ambapo jumla ya ajira 5,595 zimerekodiwa mwaka 2023. Aidha, kiwango cha ubakizaji wa bima za kawaida (general insurance retention) kimeongezeka kutoka asilimia 49.4 hadi asilimia 55.5 huku kiwango cha ubakizaji wa bima za maisha kikiwa ni asilimia 83.2.

Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, inatoa haki ya msingi ya kila Mtanzania kuwa na bima ya afya bila kujali kama wanatoka katika sekta rasmi au isiyo rasmi. Katika kutekeleza hilo TIRA imepewa jukumu la kisheria kusimamia skimu zote za bima ya afya ili kuhakikisha watoa huduma wanafuata taratibu sahihi za usajili wa wanachama na pia kufuatilia utekelezaji wa huduma zinazotolewa ili huduma zinazotolewa ziendeele kuwa bora na za haki kwa wanachama walio kwenye skimu husika. Mwaka 2024, kanuni kwa ajili ya kuanza kwa utekelezaji wa sheria hiyo zimetoka ambapo zin

asisitiza juu ya usajili wa wana chama kwa uwazi na kuhakikisha michango inawasilishwa kwa wakati.

Katika kuchangia juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya TIRA kwa kushirikiana na wadau imetoka kadi za bima ya afya 3000 kwa Watanzania wenye uhitaji ikiwa ni utekelezaji wa kauli ya Kamishna wa Bima Tanzania aliyoitoa ya kuchangia kadi za bima kwa Watanzania 10,000,000 ili waweze kupatiwa matibabu.

Elimu na ushirikiano kwa jamii

TIRA imeendelea kusimamia utoaji wa elimu ya bima kwa makundi mbalimbali ya jamii. Kupitia programu maalumu za kuelimisha, Mamlaka imefanika mikutano na wamiliki wa mabasi, waendesha bodaboda, na makundi mengine muhimu katika sekta ya usafirishaji. Hii imelenga kuwajengea uwezo wa kuelewa bima na faida zake, huku ikipunguza changamoto zinazokumba sekta hiyo.

Katika kuimarisha ufahamu wa bima kwa makundi maalumu, TIRA imekuwa mistari wa mbele kufanikisha usawa wa kijinsia na kujumuisha watu wenye mahitaji maalumu. Maonyesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Sabasaba na Nane Nane yamekuwa jukwaa la kuelimisha kuhusu bima kwa lugha nyepesi na njia zinazovutia.

Mageuzi ya kisera na kisheria

Kwa mwaka huu, TIRA imezindua miongozo na sera zinazolenaga kuboresha mazingira ya kisheria kwa watoa huduma za bima na wateja. Hii ni pamoja na kuongeza uwajibikaji wa kampuni za bima kuhakikisha fidia zinazilipwa kwa wakati. Kwa kushirikiana na taasisi za Serikali, TIRA imehakikisha kwamba mali za umma zin alindwa ipasavyo kupitia bima, hatua inayochoea uwajibikaji wa kifedha na kupunguza mzigo wa gharama kwa Serikali. Mfano wa miongozo iliyotolewa kwa mwaka 2024 ni pamoja miongozo ya bidhaa za bima, miongozo ya wakaguzi wa nje wanaohudumia sekta ya bima na muongozo wa

ukokotoaji na ukusanyaji wa tozo za ada za bima.

Bidhaa zinazokidhi mahitaji ya wateja

Mwaka 2024 pia umeshuhudia kuzinduliwa kwa huduma mpya za bima zinazolenga mahitaji ya kipekee ya wateja. Mojawapo ya mafanikio makubwa ni kuzinduliwa kwa huduma za Takafu, ambazo zinafuata misingi ya Shariah. Uzinduzi huu umeimarisha zaidi utoaji wa huduma zinazojumuisha makundi tofauti ya dini na tamaduni.

Maonesho ya kimataifa na ushirikiano kwa jamii

Katika maonesho makubwa ya Sabasaba 2024, TIRA na wadau wa sekta ya bima ilizindua "Kijiji cha Bima," ambapo wananchi walipata fursa ya kujifunza kuhusu huduma za bima kupitia njia rahisi na shirikishi. Kijiji hiki kimekuwa mfano wa ubunifu wa kuifikisha bima kwa kila mmoja, huku kikionyesha dhamira ya TIRA ya kuimarisha elimu ya bima kwa Watanzania wote.

Maono ya TIRA kwa soko salama la bima

Kwa mwaka 2024, TIRA imeendelea kuimarisha mifumo ya kidijitali inayowezesha usajili wa bima, ulipaji wa fidia kwa wakati, na usimamizi wa masuala ya kisheria kwa uwazi zaidi. Mfumo huu unalenga kujenga imani miongoni mwa wateja na watoa huduma, huku ukihakikisha ukuaji wa sekta ya bima nchini.

Kauli ya Kamishna wa Bima, Dk Baghayo Saquare

"Sekta ya bima ni nguzo muhimu kwa uchumi wa Taifa. Tunaendelea kushirikiana na wadau wote kuhakikisha huduma za bima zinawafikia Watanzania wote kwa uwazi, ubora, na ufanisi," anasema Dk Saquare.

Kwa mafanikio haya ya mwaka 2024, TIRA imeendelea kuthibitisha nafasi yake kama mshirika wa maendeleo ya Taifa. Mamlaka imeonyesha kuwa bima si tu kinga dhidi ya majanga, bali pia ni chombo muhimu cha kuboresha maisha na uchumi wa kila mtanzania.

"Sekta ya bima ni nguzo muhimu kwa uchumi wa Taifa. Tunaendelea kushirikiana na wadau wote kuhakikisha huduma za bima zinawafikia Watanzania wote kwa uwazi, ubora na ufanisi,"

Dk Baghayo Saquare, Kamishna wa Bima Tanzania.



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania
JENGO LA PSSSF, Ghorofa ya 5, Mtaa wa Makole, S.L.P 2987, DODOMA, Tanzania,
Barua pepe : coi@tira.go.tz | Simu/Nukushi
Piga Bure: +255 26 2321180 | Simu: +255 0222135137 | Nukushi: +255 26 2321180

Kama una mada yoyote inayohusu bima unataka iandikwe katika ukurasa huu kwa lengo la kuelimisha jamii usisite kuwasiliana nasi kupitia anuani yetu maoni@tira.go.tz tuma ujumbe kupitia Na. ya simu 0739 525444 TIRA: Kwa Soko Salama la Bima

INSURANCE

Matukio
kwenye
Vibango



**Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)**

UWASILISHAJI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA TANZANIA 2023/24



20 Februari
2025



Kuanzia
Saa 2:00 asubuhi



Hotel Verde,
Zanzibar

MGENI RASMI:

Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti
wa Baraza la Mapinduzi

TIRA Kwa Soko Salama la Bima

Karibuni



✉ col@tira.go.tz

🌐 www.tira.go.tz

☎ +255 222 132 537

📱 FB, IG, X: //@tira_tz



**Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)**

Miaka

61
ya
Mapinduzi

Bodi ya Taifa ya Bima, Menejimenti na Wafanyakazi wa
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania wanawatakiā
kheri ya miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

#TIRAKwaSokoSalamaLaBima



✉ col@tira.go.tz

🌐 www.tira.go.tz

☎ +255 222 132 537

📱 FB, IG, X: //@tira_tz



**Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)**

Ni Kesho! Tega Sikio Euelimike



23 Januari 2025
Kuanzia Saa 02:00 - 03:30 Asubuhi



Kipindi:
Kumepambazuka



Mada: Maendeleo Katika Sekta ya
Bima nchini

Atashiriki

Dkt. Baghayo A. Saqware
Kamishna wa Bima Tanzania

**Fuatilia
Mbashara**



✉ col@tira.go.tz

🌐 www.tira.go.tz

☎ +255 222 132 537

📱 FB, IG, X: //@tira_tz



**Mamlaka ya Usimamizi
wa Bima Tanzania (TIRA)**

Heri ya Siku ya Kuzaliwa

Bi. Khadija Said
Naibu Kamishna wa Bima Tanzania

**Tunakutakia afya njema,
furaha tele na mafanikio.**

**Tunauthamini mchango wako
katika kukuza na kuendeleza
sekta ya bima nchini.**



✉ col@tira.go.tz

🌐 www.tira.go.tz

☎ +255 222 132 537

📱 FB, IG, X: //@tira_tz



TIRA & 2025

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987

DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz

+255 26 2321180

+255 0222135137

+255 26 2321180

FB, IG, X: [@tira_tz](https://www.facebook.com/tira_tz)

www.tira.go.tz